

Maswali

1. Prisila, Akila na Paulo walikuwa wapi kabla ya kukutana Korintho?
2. Mbona Wayahudi wote walitoka Rumi?
3. Paulo, Akila na Prisila walikuwa wazuri kwa kazi gani?
4. Kazi ya Paulo ilimsaidiaje alipokuwa akisafiri?
5. Kwa mda mchache Paulo aliondoka Korintho mbona?
6. Akila na Prisila walienda wapi walipotoka Korintho?
7. Akila na Prisila waliambia Apolo nini?
8. Ndugu na dada wa Efeso walisaidiwa na Akila na Prisila namna gani?
9. Akila na Prisila walienda wapi walipotoka Efeso?
10. Akila na Prisila ni mfano mzuri kwetu namna gani?

Majibu

1. Akila na Prisila walikuwa wakiishi Rumi na Paulo alikuwa ametoka Athene.
2. Kwa sababu mfalme alikuwa amewambia watoke.
3. Akila, Prisila na Paulo walifanya kazi ya ngozi.
4. Ilimwezesha alipe nyumba za kulala.
5. Alitaka kwenda Yerusalemu kwa siku ya karamu.
6. Walienda Efeso.
7. Kufufuka kwa Yesu kulikuwa thibitisho kwamba yeye ndiye mwokozi aliyezungumziwa kwa Agano la Kale.
8. Waliwakaribisha kukutania kwa nyumba yao.
9. Walirudi Rumi.
10. Kwa sababu:
 - (1). Walikuwa na bidii kama mme na mke.
 - (2). Walipea waumini nafasi ya kukutania kwa nyumba yao.
 - (3). Walitaka kuhubiri juu ya Yesu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



49 Akila na Prisila

Marejeo

Matendo ya Mitume 18

Kiini cha somo


Tunatakiwa tutumie kila kitu tulicho nacho kusaidia wale wanaohubiri injili.

Maneno maalum

1. Rumi + fukuza + Korintho + Paulo
2. Wote Wanatengeneza hema + wanatengeneza ngozi
3. Lipa chumba cha kupanga + kijana Mfarisayo
4. Eklesia + Yerusalemu + Efeso
5. Apolo + Yohana mbatizaji + Yesu Uyunani
6. Mikutano ya nyumba + barua
7. Kosa + Rumi
8. Amani + nyumba + Yesu

49.1 Prisila na mmewe Akila walitoka Rumi na kwenda Korintho kabla Paulo naye aje kutoka Athene. Mfalme Klaudio aliambia Wayahudi wote watoke Rumi. Wayahudi hawakupendwa na watu. Kulikuwa na Wayahudi wachache kwa kila mji. Mara nyingi walilaumiwa kwa kosa lililotokea mjini. Akila na Prisila waliuliza Paulo akae nyumbani kwao. Alifurahi sana kwa ukarimu huo.

49.2 Paulo alikuwa na kazi. Biblia inasema alikuwa akitengeneza mahema - labda alifanya zaidi ya mahema. Labda alifanya kazi ya ngozi ya kutengeneza viatu na vitu vingine.



49.3 Akila na Prisila nao walifanya hiyo kazi. Kwa hivyo walisaidiana. Lazima walikuwa na mazungumzo wakati wa kazi. Labda walizungumza juu ya Mungu na mwanawe Yesu Kristo. Hiyo kazi yake ilimsaidia kulipa vyumba vya kulala popote alienda. Aliuza vitu alivyotengeneza akipata pesa. Paulo hakutaka kitu chochote bure. Alijifunza kufanya hii kazi wakati alikuwa mdogo. Vijana wa Mafarisayo walijifunza kazi ili wasitegemee watu wengine.

49.4 Kwa mda Paulo alikaa Korintho kwa hivyo alianzisha eklesia huko. Tunaona kwa Biblia aliwandikia barua mbili. Baadaye Paulo aliamua kurudi Yerusalemu kuona kanisa la huko. Akila na Prisila walienda naye. Walipita njia ya Efeso na Akila na Prisila wakabaki hapo. Wakamngojea Paulo kule. Walipokuwa wakingojea, walikutana na Muyahudi aliyetwa Apolo.

49.5 Apolo alikuwa mhubiri wa ajabu. Kila mtu alimsikiliza akinena. Alijua unabii wa Agano la Kale uliozungumzia Masiya atakayekuja. Alikuwa amebatizwa na Yohana mbatizaji. Alizungumza juu ya Yesu lakini hakujua kufufuka kwake. Akila na Prisila walimkaribisha kwa nyumba yao na wakamwambia yote kuhusu Yesu. Alielewa yote aliyofanyiwa na Yesu. Akataka kwenda Uyunani. Ndugu wa Efeso walifurahi kumtuma kule. Alipofika kule alifanya kazi kwa bidii akisaidiana na ndugu na dada.

49.6 Baada ya mda, Paulo alirudi Yerusalemu kutoka Efeso. Eklesia walikutania kwa nyumba ya Akila na Prisila. Labda Paulo aliishi na kufanya kazi nao tena. Aliishi Efeso kwa miaka miwili hata akaandikia eklesia mpya ya Korintho barua akiwa huko.



49.7 Kukaa kwa Paulo Efeso kulikatishwa. Kulikuwa na watu wengi waliomlelea shida kwa hivyo aliamua kurudi Korintho. Akila na Prisila nao walirudi Rumi hata anapoandikia eklesia ya Rumi anawatumia salamu.

49.8 Akila na Prisila ni mfano mzuri kwetu wakati huu. Walikuwa wa bidii kama mme na mke. Kwa maandiko matakatifu majina yao yanapatikana pamoja. Makasi yao walikoishi waumini walikutania kule. Popote walienda, walipenda kuhubiria watu juu ya Yesu.